/ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 30 ***11th August, 2023***

SUBSIDIARY LEGISLATION

To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 30 Vol. 104 Dated 11th Aug, 2023
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 575 la tarehe 11/8/2023

SHERIA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA NA 272)

_____

AMRI

_____

(Imetolewa chini ya Kifungu cha 29 (1)(d))

AMRI YA KUREKEBISHA BEI YA MAMLAKA YA USAMBAZAJI MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MAKONDE PLATEAU (MAKONDE PLATEAU WSSA) YA MWAKA 2023

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Bei ya Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya Makonde Plateau (Makonde WSSA) ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei na ada za Makonde WSSA zinarekebishwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitazingatia masharti yafuatayo;

(a) Makonde WSSA, kabla ya kutoa ankara kwa kutumia bei na ada zilizoainishwa kwenye Amri hii, itapaswa kuwasilisha uthibitisho kwa EWURA kwamba iliwataarifu wateja wake kuhusu amri mpya ya bei na kwamba iliwafahamisha ipasavyo wadau wake ikiwa ni pamoja na viongozi wa serikali, kisiasa, dini na wateja wake, kuhusu mabadiliko ya bei;

(b) Makonde WSSA itawasilisha EWURA mnamo

au kabla ya tarehe 30 Septemba 2023, mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(c) Makonde WSSA itahakikisha kuwa, mnamo au kabla ya tarehe 31 Agosti 2023, inawasilisha malipo ya ada ya udhibiti kiasi cha Shilingi 17,476,990.21 kwa mujibu wa kumbukumbu za tarehe 21 Juni 2023;

(d) Makonde WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(e) Makonde WSSA itahakikisha kuwa, mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2024, inafikisha huduma ya maji karibu na taasisi za umma (vituo vya afya, zahanati na shule) ili kutoa urahisi kwa taasisi hizo kuunganishwa na huduma za maji;

(f) Makonde WSSA itahakikisha inatoa huduma ya maji kwa wakazi wote waishio kandokando ya vyanzo vya maji mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2025;

(g) Makonde WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kutoa elimu kwa wateja wake na kuwasilisha EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(h) Makonde WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu;

(i) Makonde WSSA kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(j) Makonde WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na hali ya utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Makonde

WSSA, ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji safi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake;

(k) Makonde WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua, ili kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususan kipindi cha kiangazi.

Utenguzi wa Amri TS Na. 145 ya Mwaka 2019

4. Amri hii inafuta Amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 15 Februari 2019.

_____

JEDWALI LA KWANZA

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

Makundi ya Wateja	Bei za Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2020/21	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	1,400	2,341	2,394	2,481
Taasisi	1,500	2,509	2,565	2,659
Biashara	1,600	2,676	2,736	2,836
Viwanda	1,900	3,178	3,249	3,368
Wateja Wakubwa	1,000	1,672	1,710	1,772
Maboza	5,000	8,362	8,551	8,862
Magati	1,000	2,000	2,000	2,000
Wastani	1,274	2,131	2,180	2,259

Jedwali Namba 1(b): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Unganisho)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho	26,000	26,000	26,000
Taasisi		26,000	26,000	26,000
Biashara		26,000	26,000	26,000
Viwanda		26,000	26,000	26,000

Jedwali Namba 1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi kwa Rejesho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa na Makonde			Ada Zilizoidhinishwa		
		2023/24	2024/25	2025/26	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	50,000	50,000			15,000	15,000	15,000
Taasisi					15,000	15,000	15,000
Biashara					15,000	15,000	15,000
Viwanda					15,000	15,000	15,000

_____

JEDWALI LA PILI

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3 (d)))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Miradi Itakayotekelezwa	Gharama (TZS)		
	2023/24	2024/25	2023/24
UWEKEZAJI MPYA			
Ununuzi na ufungaji wa vipuri (sluice valve/gate valve) DN 32, 50, 75, 100 na 100) kwa ajili ya upanuzi wa mtandao ifikapo Juni 2026	5,000,000	10,000,000	20,000,000
Manunuzi ya bomba na viungio kwa ajili ya upanuzi wa km70 za mtandao kwenye maeneo yasiyofikiwa na huduma (Masaki, Namikupa, Kitama, Chikongola, Malopokelo, Legeza, Mji Mpya, Amkeni, Mmovo, Mkunya, Mtangalanga, Nambunga, Julia, Mkulung'ulu, Majengo na Kitangari Sokoni)(yakiwemo maeneo ya taasisi za umma na huduma) kwa kutumia bomba za kipenyo cha mm 32 hadi mm 110 ikihusisha uchimbaji na ufukiaji wa mitaro; km 20 (2023/24); km 25 (2024/25); km 25 (2025/26)	343,000,000	521,600,000	603,300,000
Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya maabara kwa ajili ya uchunguzi na ufuatiliaji wa viashiria vya ubora wa maji	10,000,000	12,000,000	15,000,000
Ununuzi wa ekari 5 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi	15,000,000	15,000,000	15,000,000
Jumla ya Gharama za Uwekezaji Mpya	373,000,000	558,600,000	653,300,000
MIRADI YA UKARABATI			
Manunuzi na kubadilisha mita chakavu 3,000	136,000,000	163,000,000	196,000,000

Tangazo la Serikali Na.575 (Linaendelea.)

Miradi Itakayotekelezwa	Gharama (TZS)		
	2023/24	2024/25	2023/24
Kununua bomba mpya na viungia kwa ajili ya kubadilisha km 10 za bomba chakavu za kipenyo cha kuanzia mm 50 hadi mm 110 ikiwemo uchimbaji na ufukiaji wa mtaro	20,000,000	35,000,000	40,000,000
Kununua na kubadilisha vifaa chakavu vya bomba sluice valve 20 za kipenyo cha mm 100 hadi mm 160; 8 kwa mwaka 2023/24, 7 kwa mwaka 2024/25 na 5 kwa mwaka 2025/26	4,800,000	4,200,000	3,000,000
Kununua na kubadilisha mita kuu 18 kwenye mitambo ya uzalishaji na usambazaji maji; 5 kwa mwaka 2023/24, 5 kwa mwaka 2024/25 na 8 kwa mwaka 2025/26 za vipenyo kuanzia mm 80 hadi mm 150.	2,200,000	2,200,000	3,700,000
Jumla ya miradi ya ukarabati	163,000,000	204,400,000	242,700,000
JUMLA YA UWEKEZAJI WOTE	536,000,000	763,000,000	896,000,000

_____

JEDWALI LA TATU

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3 (h)))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Maelezo	Kizio	Lengo la Utendaji		
		2023/24	2024/25	2025/26
Idadi ya watu inayofikiwa na huduma ya maji	%	85	90	95
Maunganisho mapya ya majisafi	No	1,000	1,000	1,000
Upotevu wa Maji	%	45	30	20
Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja	%	100	100	100
Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato	%	92	95	97

_____

JEDWALI LA NNE

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3 (i)))

MAPATO YANAYOHITAJIKA

Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato (TZS)			
Maelezo	Makisio		
	2023/24	2024/25	2025/26
Gharama za Uzalishaji	635,478,071	637,260,988	834,142,015
Gharama za Usambazaji	246,502,636	246502636	246502636
Ukarabati na Matengenezo	159,595,669	510,706,142	1,634,259,665
Gharama za Kiutumishi	415,465,893	476,857,761	582,365,128
Gharama za Kiutawala	250,493,244	287,888,534	358,129,800
Gharama za Matangazo	22,575,000	23,703,750	24,888,938
Gharama za Matukio na Ufadhili	19,036,750	19,416,588	19,815,417
Gharama za Utunzaji wa Fedha	516,240	516,240	516,240
Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo	1,749,663,504	2,202,852,638	3,700,619,838
Ukarabati na Kubadili Miundombinu	163,000,000	204,400,000	242,700,000
Uwekezaji wa Miundombinu Mipya	373,000,000	558,600,000	653,300,000
Mapato Yote Yanayohitajika (000´TZS)	2,285,663,504	2,965,852,638	4,596,619,838
Ondoa:			
Mapato Mengineyo	29,900,000	29,900,000	29,900,000
Mapato Kutokana na Mauzo ya Maji	2,255,763,504	2,935,952,638	4,566,719,838

Dodoma,
..... 2023

JAMES A. MWAINYEKULE,
Mkurugenzi Mkuu